**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Simu Nambari: 2152532/3
Fax Na: 2152820
*(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe Kwa Kamishna wa Mamlaka)*

8 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 80327,
**DAR ES SALAAM.**

# TAARIFA KWA UMMA

## DAWA ZA KULEVYA ZATEKETEZWA

**Dar es Salaam, Oktoba 08, 2019.**

Leo tarehe 08 Oktoba 2019, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mahakama, Jeshi la Polisi, Idara ya Usalama wa Taifa, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Baraza la Taifa la Mazingira imefanya uteketezaji wa dawa za kulevya ambazo kesi zake zimeshahukumiwa.

Dawa hizo zinahusiana na kesi zilizomalizika katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Mkoani Dar es Salaam. Jumla ya dawa za kulevya zilizooteketezwa ni **kilo 120.91 au (120,919.88 gramu**) za **Heroin** na **kilo 70.96 (70,967.86 gramu) za Cocaine** zinazohusha kesi 35. Aidha, uzito wa dawa hizo unajumuisha **Kilo 63.155 za Heroin** ambazo kesi yake imehukumiwa tarehe 27/09/2019 mkoani Mtwara ikimuhusisha **Mwinyi Kitwana Rajabu na Ally Hamdan Hamad** na kushindwa kuziteketezea mkoani humo.

Uteketezwaji huu umefanyikia katika kiwanda cha saruji cha Twiga kilichopo eneo la Wazo Hill jijini Dar es Salaam. Hii ni mara ya kwanza uteketezwaji wa dawa za kulevya kufanyika tangu kuanza kwa mwaka huu wa 2019 kwa mkoa wa Dar es Salaam, ambapo mara ya mwisho uteketezaji kama huu ulifanyika mwaka 2015 katika kiwanda cha saruji cha Twiga na ulihusisha uteketezaji wa Dawa za Kulevya aina mbalimbali.

Kwa mujibu wa sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, ili dawa za kulevya ziteketezwe lazima kuwepo na amri ya Mahakama iliyosikiliza kesi na kumalizika au ambapo kesi hiyo ipo. Pia uteketezaji wa dawa za kulevya hufanyika kwa utaratibu maalumu ili kuepuka uharibifu wa mazingira na madhara ya kiafya kwa wananchi hivyo viwanda vya saruji hutumika.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inatoa rai kwa watanzania kushiriki kikamilifu katika kutoa taarifa za wazalishaji, wafanyabiashara na watumiaji wa Dawa za Kulevya. Pia inaiasa jamii kutojihusisha biashara na matumizi ya dawa hizi.

Imetolewa na,

L. B. Matho

Afisa Habari

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.